Tangazo la Serikali Na.1004 (Linaendelea.)

TANGAZO LA SERIKALI Na. 1004 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

_____

NOTISI

_____

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA NYANGEDI KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA NYANGEDI YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Nyangedi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyangedi ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyangedi.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyangedi ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, uwanda wa nyasi na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa

maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyangedi.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu wa Nyangedi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyangedi, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

Tangazo la Serikali Na.1004 (Linaendelea.)

_____

JEDWALI

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

WILAYA YA LINDI

MSITU WA HIFADHI YA TAIFA NYANGEDI

Makadirio ya eneo: Hekta 4501.199 au Kilometa za Mraba 45.01 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Nyangedi unaopatikana Wilaya ya Lindi katika Mkoa wa Lindi kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3123 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:



Dodoma,
....., 2024

PNIDI HAZARA CHANA,
Waziri wa Maliasili na Utalii